



# LONDA

RIPOTI YA HAKI ZA KIDIJITALI NA USHIRIKSHWAJI KATIKA AFRIKA

TOGO



# LONDA

**Ripoti ya Haki za Kidijitali na Ushirikishwaji Barani Afrika 2022**

Imechapishwa na Paradigm Initiative  
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria  
Email: [media@paradigmhq.org](mailto:media@paradigmhq.org)  
[www.paradigmhq.org](http://www.paradigmhq.org)

Iliyochapishwa Aprili 2023

Ripoti iliyotolewa na Paradigm Initiative  
Ubunifu na Muundo na Kenneth Oyeniya

Chapisho hili linaweza kunaswa tena kwa matumizi yasiyo ya kibiashara kwa namna yoyote ile mradi sifa inayostahili imetolewa kwa wachapishaji, na kazi itawasilishwa bila upotoshaji wowote.

Hakimiliki © 2023 Paradigm Initiative



Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)

ISBN: 978-978-797-8980-8



# Togo

## ► Ufupisho

Kwa Watogo wengi, upatikanaji wa huduma za umma, za kibinafsi na za kijamii ni changamoto. Serikali inaangazia njia moja anayoweza kutoa suluhu ambayo ni mpango wake kabambe wa kitambulisho cha kibayometriki wa E-ID Togo na mpango wa hivi karibuni wa kuunganisha nchi kwenye kebo ya Google ya Equiano, wa kwanza wa aina yake kufika Afrika kutoka Ureno unaotarajiwa kuongeza kasi ya intaneti maradufu kwa wakazi milioni 8.9 wa Togo. Google ilisema kuwa mtandao huo utafungua kwa njia isiyo ya moja kwa moja nafasi za kazi 37,000 nchini Togo kufikia 2025 na kuongeza Pato la Taifa kwa \$193 milioni <sup>1</sup>. Pia, Togo imekuwa nchi ya kwanza Afrika Magharibi kuzindua mtandao wa 5G mnamo 2020. Katika miaka ya hivi karibuni, kupatikana kwa mtandao nchini Togo kumeongezeka karibu mara tatu, kutoka karibu asilimia 7 mwaka 2017 hadi karibu asilimia 21 mwaka wa 2020<sup>2</sup>. Hata hivyo, vyombo vya siasa na uhuru wa kujieleza wa watu na vyombo vya habari bado ni changamoto. Pamoja na kwamba serikali imezindua miradi kabambe yenye lengo la kuongeza ajira zaidi kupitia ujuzi wa kidijitali na kuunganishwa, TEHAMA bado haijaingizwa katika programu za elimu nchini na sera na programu zilizobuniwa na serikali hivi karibuni hazina ushiriki wa wahusika wakuu kama vile asasi za kiraia, Jumuiya za kiufundi na wasomi.

<sup>1</sup> *The Equiano Subsea Cable has arrived in Togo, first stop in Africa (2022)* Official Google Africa Blog. Available at: <https://africa.googleblog.com/2022/03/the-equiano-subsea-cable-has-arrived-in.html> (Accessed: January 25, 2023).

<sup>2</sup> *BTI 2022 Togo Country Report (2022)* BTI. Available at: <https://bti-project.org/en/reports/country-report/TGO> (Accessed: January 25, 2023).



## Utangulizi

Togo inapatikana Afrika Magharibi kwenye Ghuba ya Guinea, imepakana na Ghana upande wa magharibi, mashariki na Benin na kaskazini na Burkina Faso. Ikiwa katikati ya nchi hizi, nchi ya Togo ina aina mbalimbali za lugha, historia changamano ya kidini na inasifika kwa chakula kitamu.

Idadi kubwa ya wakazi wa Togo wanaishi katika vijiji vidogo vilivyotawanyika katika maeneo ya mashambani. Lomé, ni mji mkubwa zaidi, unapatikana kando ya pwani. Moja ya madini muhimu zaidi ya Togo ni phosphate, na nchi ina takriban tani milioni 60 katika hifadhi, na kufanya taifa hilo la Afrika Magharibi kuwa la 19 kwa uzalishaji mkubwa wa madini duniani. Nchi pia ina rasilimali mbalimbali ambazo hazijatumiwa kama uzalishaji wa madini kama chokaa, dhahabu, na almasi, chuma, jasi, bauxite, manganizi, zinki, rutile, na zaidi <sup>3</sup>.

Bei za chini za soko za bidhaa kuu za Togo zinazouzwa nje, hata hivyo, pamoja na hali tete ya kisiasa ya miaka ya 1990 na mwanzoni mwa miaka ya 2000, zilikuwa na athari mbaya kwa uchumi. Rais wa Togo, Faure Gnassingbe, alichaguliwa tena kwa muhula wa nne mnamo 2020, akiongeza utawala wake wa miaka 15 na uongozi wa kifamilia ambao ulianza wakati wa baba yake alipochukua mamlaka katika mapinduzi ya 1967. Ingawa katiba inatoa uhuru wa kusema, kiutendaji haki hiyo imewekewa vikwazo, na mara nyingi waandishi wa habari hujidhibiti.

Idadi ya jumla ya watu nchini ilikuwa milioni 8.9 mnamo Desemba 2022<sup>4</sup>. Kulingana na data ya Kepios, idadi ya watu wa Togo iliongezeka kwa 201 elfu kati ya 2021 na 2022<sup>5</sup>. Mwanzoni mwa 2022, asilimia 43.9 ya wakazi wa Togo waliishi mijini, huku asilimia 56.1 wakiishi vijijini.

Uchambuzi wa Kepios unaonyesha kuwa watumiaji wa intaneti nchini Togo waliongezeka kwa 259 elfu kati ya 2021 na 2022. Kwa mtazamo, takwimu hizi za watumiaji zinaonyesha kuwa watu milioni 6.35 nchini Togo hawakutumia intaneti mwanzoni mwa 2022, kumaanisha kuwa asilimia 74.1 ya watu walibaki nje ya mtandao mwanzoni mwa mwaka.

Mnamo Novemba 2022, Togo ilikuwa kwenye kurasa za mbele za karibu magazeti yote ya teknolojia na mawasiliano kote ulimwenguni kwa kuwa nchi ya kwanza ya Kiafrika kuunganishwa na kebo ya The Equiano ya Google, ya kwanza ya aina yake kufika Afrika.

"Togo, ambayo haikuwa katika orodha ya nchi zilizonufaika za kundi la kwanza, iliunganishwa baada ya miezi kadhaa ya mazungumzo na inakuwa nchi ya kwanza ya Kiafrika kuwa mwenyeji wa kebo," aliongea

3 *Natural Resources & Mining Industry in Togo (2022) Arise IIP*. Available at: <https://www.ariseiip.com/natural-resources-mining-industry-in-togo/#:~:text=Phosphate%20mining%20is%20a%20major,of%20minerals%20in%20the%20world> (Accessed: January 25, 2023).

4 *Togo population (live) (2023) Worldometer*. Available at: <https://www.worldometers.info/world-population/togo-population/> (Accessed: January 25, 2023).

5 Kemp, S. (2022) *Digital 2022: Togo - DataReportal - global digital insights*, DataReportal. DataReportal - Global Digital Insights. Available at: <https://datareportal.com/reports/digital-2022-togo#> (Accessed: January 25, 2023).

# Uchambuzi wa Nchi

Waziri wa Togo wa Uchumi wa dijitali na Mabadiliko ya Digi, Cina Lawson, , mnamo Machi 18, kwenye gati ya bandari inayojiendesha ya Lomé (Togo Terminal).

“Mafanikio haya yanatuwezesha kukidhi mahitaji ya mpango wa serikali juu ya kuimarisha muunganisho wa intaneti kwenye mtandao wa kimataifa,” aliongeza waziri wa Togo. Kebo hiyo, “ambayo lazima itoe mara 20 ya kipimo cha data cha kebo nyingine yoyote iliyopo Afrika Magharibi”, ni sawa na ongezeko la kasi ya intaneti, kuboresha kwa watumiaji wenye uzoefu, na kupunguzwa kwa gharama za data kwa zaidi ya 14% ifikapo 2025, kulingana na data kutoka kwa wizara yake.

Mnamo 2020, katikati ya janga la UVIKO-19, Togo ikawa nchi ya kwanza Afrika Magharibi, na ya tatu barani Afrika, kupokea mtandao wa 5G. Akizungumzia uzinduzi huo wa kushtukiza, Waziri wa Uchumi wa Kidijitali na Mabadiliko ya Kidijitali, Cina Lawson, alisema: “5G itarahisisha matumizi ya kibunifu kwa kuruhusu kuibuka kwa huduma mpya zinazokidhi mahitaji ya sekta mbalimbali za uchumi (nishati, afya, viwanda, usafirishaji, nk).

Kwa kuongezea, lengo la serikali ni mawasiliano ya simu kuwanufaisha Watogo wote. Kwa hiyo ni muhimu kuhakikisha kwamba utumiaji wa teknolojia hii hauishii tu kwa miji mikubwa pekee, bali unachangia kuboresha ubora wa huduma ili maeneo yote nchini Togo kufaidika na huduma za 5G.”

Pia, katikati ya janga la UVIKO-19, Togo kupitia Wizara ya Uchumi wa Kidijitali na Mabadiliko ya Kidijitali (MENTD) ilizindua mpango wa kuhamisha pesa wa Novissi. Mpango wa uhamishaji pesa bila masharti (UCT) kusaidia wafanyakazi wasio rasmi ambao maisha yao yamepata changamoto kutokana na janga la coronavirus,

Novissi ni mpango kamili wa usaidizi wa kijamii wa kidijitali. Kufikia Machi 2021, mpango wa Novissi ulikuwa umefikia wanufaika 819, 972 na kutoa takriban Dola za Marekani milioni 23.9 (13,308,224,040 FCFA). Mpango huo ulisifiwa kote ulimwenguni kama hatua kubwa ya utekelezaji wa uchumi wa kidijitali na usaidizi wa kijamii wakati wa majanga.

Kwa vichwa hivi vya habari, mtu aliye nje ya uchumi wa nchi anaweza kufikiria kuwa nchi imebuni ramani ya kidijitali na mchakato wa wazi wa kuunda sera ambao zinaleta wahusika pamoja ili kupunguza mgawanyiko wa kidijitali. Walakini, mchakato huu umeonyesha ukomo wake kwani watu wengi nje ya jiji kuu bado wanatatizika kuunganishwa na mitandao ya 2G wakati nchi inazindua mtandao wa 5G na mradi kabambe wa akili bandia (AI) bila mfumo uliopo wa kisheria na udhibiti unaofaa kwa mifumo ya teknolojia hizi.

## SERA YA LEAPFROG DHIDI YA MCHAKATO WA SERA YA WASHIKADAU WENGI

Mapema miaka ya 2010, ripoti ya Taasisi ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu ilieleza kuwa kutokuwepo kwa mchakato ya maendeleo ya sera kulitokana na kukosekana kwa utulivu wa kisiasa katika taifa hilo la Afrika Magharibi.<sup>6</sup> Baada ya marekebisho ya katiba mwaka 2002 na uchaguzi wa rais mwaka 2003, nchi iliingia katika machafuko ya kisiasa.

Mwaka 2005, Jumuiya ya kimataifa na mashirika ya kikanda yalihakikisha makubaliano ya kugawana madaraka, ambayo yalidumu hadi 2007 wakati serikali ilibadilishwa mara mbili na mawaziri wapya. Majaribio ya kushirikisha serikali kuunda sera ya Tehama yalikabiliwa na hatari kubwa, ingawa mkataba wa kisiasa wa Togo uitwao Accord Politique Global (APG) ulitiwa saini katika nchi jirani ya Burkina Faso mnamo Agosti 2006, kufuatia mazungumzo kati ya serikali na vyama mbali mbali vya upinzani.

Ilikuwa karibu isiwezekane, chini ya hali ya machafuko ya kisiasa nchini Togo mapema miaka ya 2000 kutilia maanani masuala ya sera ya TEHAMA, licha ya majaribio ya kufanya hivyo.

Vile vile, ilikuwa vigumu pia kushirikisha serikali na mipango inayoendelea ya sera za kitaifa na kikanda kama ile iliyoongozwa na Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa ya Afrika (UNECA) chini ya mpango wa Taifa wa Miundombinu ya Habari na Mawasiliano (NICI) na Jumuiya ya Kiuchumi ya Magharibi Nchi za Afrika (ECOWAS) mageuzi ya ICT. Kwa jumla zaidi ya majaribio 10 yamefanywa kutoa waraka wa kitaifa wa sera ya tehama bila kuleta matokeo

6 “Supporting Multistakeholder Internet Public Policy Dialogue in a Least Developed Country: The Togo Experience,” Ben Akoh, *International Institute for Sustainable Development*, July 2012.

yanayoonekana.

Hata hivyo, Waziri wa sasa wa Uchumi wa Kidijitali na Mabadiliko ya Kidijitali amekuwa katika nafasi hiyo tangu 2010. Kutokana na uzoefu wake wa zaidi ya miaka 15 na utaalamu katika sera na udhibiti wa mawasiliano ya simu, alipewa jukumu la kuiongoza Togo kupitia mpito mkubwa hadi uchumi wa kidijitali jumuishi. .

Vilevile, mipango mingi, ikiwa ni pamoja na sheria na kanuni katika kipindi cha miaka 12 ya uongozi wa wizara, imetengwa kwa kasi ya sera ya leapfrog bila msingi madhubuti wa kujenga mchakato wa sera za wadau mbalimbali unaojumuisha wahusika wakuu kama vile watumiaji wanaowakilishwa na Mashirika ya Kiraia, jumuiya ya kiufundi na wasomi. Usiri wa mchakato na ukosefu wa uwajibikaji, ushirikishwaji na uwazi ni viashiria vikubwa kwamba sera nyingi zinazoendeshwa na Serikali kupitia wizara hiyo si lazima ziweke misingi imara ya uchumi wa kidijitali wa nchi bali ni kwa sababu ya wasiwasi. kurekebisha sera za serikali kwa mazingira ya kimataifa ya kidijitali wakati wa uongozi wao kama maafisa wa serikali.

Sera ya hivi majuzi zaidi iliyohusu mpango wa Novissi<sup>7</sup> ilitungwa na mawaziri pekee na mshauri kutoka Ofisi ya Urais. Novissi iliharakishwa kupitia mazungumzo ya kawaida ya bajeti na sera na timu ya ndani iliyojitolea, iliyoongozwa na Mshauri Mkuu wa Kiuchumi wa rais, na Waziri wa Uchumi wa Kidijitali na Mabadiliko ya Dijitali. Wote wawili walifanya kazi na kamati ya dharura ya mawaziri, ambayo ilirasimishwa kupitia amri ya rais kuratibu majibu ya sera ya dharura kwa janga hili.

Kamati inaundwa na viongozi wafuatao: Rais wa Jamhuri; Waziri Mkuu; Waziri wa Uchumi wa Kidijitali na Mabadiliko ya Kidijitali; Waziri wa Maendeleo ya Machinani, Kazi za Mikono na Vijana; Waziri wa Uchumi na Fedha; Waziri wa Tawala za Mikoa, Ugotuaji na Serikali za Mitaa; Waziri wa Miundombinu na Uchukuzi; Waziri wa Madini na Nishati; Waziri wa Maji, Vifaa Vijijini na Maji; Katibu mkuu Sekta Isiyo rasmi; na Mshauri wa Rais wa Jamhuri.

Kamati ilihakikisha kwamba Novissi inaendelezwa ndani ya chombo na mchakato huu wa kitaasisi, na kuakisi vipaumbele vya usaidizi wa kijamii vya serikali. Tena, serikali ilishindwa kujenga timu ya

wadau mbalimbali yenye wataalamu wa fani hiyo na wadau wengine muhimu.

Kamati ilihakikisha kwamba Novissi inaendelezwa ndani ya mamlaka hii husika na mchakato huu wa kitaasisi, na kuakisi vipaumbele vya usaidizi wa kijamii vya serikali. Kwa mara nyingine, serikali ilishindwa kujenga timu ya wadau mbalimbali yenye wataalamu wa fani hiyo na wadau wengine muhimu.

Uhuru wa Mtandao na changamoto za kimtandao Usumbufu wa mtandao, ufuatiliaji wa serikali na matumizi mabaya ya data ya kibinafsi ya raia umeiweka Togo kipaumbele kati ya 2017 na 2021. Mwaka wa 2022 umekuwa dhabiti katika suala la uhuru wa mtandao kando na kesi chache ambapo washawishi kadhaa wa wavuti walifungwa kwa maoni yao mtandaoni. kwa kukosekana kwa mfumo wa kisheria unaodhibiti uhuru wa kujieleza mtandaoni.

Usumbufu wa mtandao, ufuatiliaji wa serikali na matumizi mabaya ya data binafsi ya raia umeiweka Togo katika nafasi ya kuangaliwa zaidi kati ya 2017 na 2021. Mwaka wa 2022 umekuwa dhabiti katika suala la uhuru wa mtandao kando na kesi chache ambapo washawishi kadhaa wa mtandaoni walifungwa kwa maoni yao mtandaoni. kwa



<sup>7</sup> Using AI and digital data to target cash transfers in Togo (2021) CEGA. Available at: <https://cega.berkeley.edu/research/using-ai-and-digital-data-to-target-cash-transfers-in-togo/> (Accessed: January 25, 2023).

kukosekana kwa mfumo wa kisheria unaodhibiti uhuru wa kujieleza mtandaoni.

Mwishoni mwa 2021, mwanaharakati wa demokrasia Fovi Katakou<sup>8</sup> pia aliachiliwa kwa muda chini ya usimamizi wa mahakama baada ya siku tisa za kizuizini. Alishtakiwa kwa “msamaha kwa uhalifu na makosa” (Kifungu cha 552 cha Kanuni ya Adhabu ya Togo) na “uchochezi wa kuasi mamlaka ya Serikali” (Kifungu cha 495 cha Kanuni hiyo) kuhusiana na chapisho la Facebook la tarehe 10 Desemba, 2021 ambapo alionya kuhusu matatizo ya ukosefu wa usalama, ukosefu wa haki, na ukosefu wa miundombinu nchini Togo.

Mwaka 2022, Aristide Soglo, almaarufu Aristo le Blédard, mfuasi maarufu wa Kifaransa-Togo alikamatwa mara kwa mara na kuhukumiwa mara kadhaa pamoja na kulipa faini kwa maoni yake aliyoyotoa mtandaoni<sup>9</sup>. Alishtakiwa kwa kukashifu na kutokana na kukosekana kwa sheria inayodhibiti uhuru wa kujieleza mtandaoni nchini Togo, mwelekeo mkuu wa polisi wa mahakama (DCPJ) umekuwa ukitumia Kanuni za Jinai za Togo.

Watu wenye ushawishi na wanablogu wakiwemo Raoul Le Blanc<sup>10</sup>, mchekeshaji maarufu, Gogoligo, na msanii wa nyimbo za injili, Papson Moutité, wamefungwa kwa kutoa maoni yao kwenye mitandao ya kijamii, haswa Facebook.<sup>11</sup>

Miaka miwili iliyopita, katika kesi ya kihistoria, Mahakama ya Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS) iliagiza serikali ya Togo “kutunga na kutekeleza sheria, kanuni na ulinzi ili kutimiza wajibu wake kuhusu haki. uhuru wa kujieleza mtandaoni kwa mujibu wa sheria za kimataifa za haki za binadamu” na “kuchukua

hatua zote zinazohitajika ili kuhakikisha kutotokea kwa usumbufu wa mtandao na matumizi mabaya ya uhuru wa Raia wa kujieleza.”

Mwanzoni mwa mwaka 2022, Baraza la Mawaziri lilipitisha kanuni mpya ya utaratibu wa uhalifu<sup>12</sup>, rasimu ya muswada wa vifungu 1047 “ili kuleta usasa zaidi katika utaratibu wa kesi za kihalifu wa Togo au kukabiliana na changamoto mpya kama vile ugaidi au uharamia wa baharini.” Kwa mujibu wa serikali, mswada huo mpya utafikia viwango vikuu vya kimataifa katika suala la uhuru wa mtu binafsi na ulinzi wa utu wa mtu binafsi. Hata hivyo, haijulikani ikiwa masharti ya uhuru wa mtandaoni yamejumuishwa katika mswada mpya. Kwa kukosekana kwa mikutano ya hadhara na wito wa kutoa maoni, bado haiwezekani kwa wadau wengine kuleta mchango wao katika muswada huo. Kuhusu kukatizwa kwa mtandao, Watu wa Togo wamefurahia utulivu wa mtandao kwa wakazi waishio mijini isipokuwa matukio machache ya pekee<sup>13</sup> ambayo yalitatuiliwa ndani ya saa au siku moja. Matukio mengi yalikuwa ni Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (ARCEP) imefungua utaratibu wa kuiwekea vikwazo GVA Togo, mtoa huduma wa mtandao wa fiber optic (ISP) kufuatia usumbufu ulioripotiwa mara kadhaa kwenye mtandao wake<sup>14</sup>. ARCEP ilishutumu ISP kwa “kutofuata majukumu ya uthabiti wa mtandao, upatikanaji na mwendelezo wa huduma” na pia kwa kushindwa kutoa taarifa mapema zinapotokea changamoto za kimtandao au miundombinu kwa wateja wake na mdhibiti.

“Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (ARCEP) imebaini kwa masikitiko kwa wiki kadhaa, mapungufu makubwa na ya mara kwa mara katika utoaji wa huduma na

8 HAKA, A. (2021) Togo-L'activiste Fovi Katakou arrêté chez lui dans la matinée, Icilome. Available at: <https://icilome.com/2021/12/togo-lactiviste-fovi-katakou-arrete-chez-lui-dans-la-matinee/> (Accessed: January 25, 2023).

9 KAMAKO, B.L. (2021) Aristo le Blédard gardé à vue par la police togolaise pour diffamation, Togo Breaking News. Available at: <https://togobreakingnews.info/aristo-le-bledard-garde-a-vue-par-la-police-togolaise-pour-diffamation/> (Accessed: January 25, 2023).

10 News, B.T.B. (2022) Showbiz: Raoul le blanc encore jeté en prison, Togo Breaking News. Available at: <https://togobreakingnews.info/showbiz-raoul-le-blanc-encore-jete-en-prison/> (Accessed: January 25, 2023).

11 News, B.T.B. (2021) Papson et gogoligo en prison dans l'affaire adebayor, Togo Breaking News. Available at: <https://togobreakingnews.info/papson-et-gogoligo-en-prison-dans-laffaire-adebayor/> (Accessed: January 25, 2023).

12 LOMEGRAPH (2022) Le Togo va introduire le bracelet électronique à son code de procédure pénale, Available at: <https://lomegraph.com/code-de-procedure-penale-bracelet-electronique/> (Accessed: January 25, 2023).

13 Ayi Renaud Dossavi (2022) Togo : L'ARCEP lance une procédure de sanction contre Canalbox, suite à des dysfonctionnements Récurrents, Togo First - Actualité économique au Togo. Available at: <https://www.togofirst.com/fr/telecoms/0309-10538-togo-l-arcep-lance-une-procedure-de-sanction-contre-canalbox-suite-a-des-dysfonctionnements-recurrents> (Accessed: January 27, 2023).

14 Agence Ecofin (2022) Au Togo, Canalbox Visé par une procédure de sanction conduite par l'arcep, pour dysfonctionnements récurrents, Agence Ecofin. Available at: <https://www.agenceecofin.com/communication/0409-100852-au-togo-canalbox-vise-par-une-procedure-de-sanction-conduite-par-l-arcep-pour-dysfonctionnements-recurrents> (Accessed: January 27, 2023).

kampuni ya Groupe Vivendi Africa Togo (GVA Togo), hususan kuzidisha kwa kesi za kutopatikana kwa huduma. na kasi ndogo zaidi chini ya Mbps 1 badala ya kasi iliyosajiliwa na watumiaji wa 50 Mbps na 200 Mbps," ilisema taarifa.


GVA Togo imekuwa msaada mkubwa wa utoaji wa huduma za kimtandao nchini Togo, ikitoa usajili wa bei nafuu zaidi wa mkongo wa mtandao ndani ya ECOWAS. ISP iliongeza wateja wake mara mbili kutoka karibu 18,000 hadi 36,000 mwishoni mwa Desemba 2021, dhidi ya hali ya nyuma ya ukuaji wake tangu kuwasili kwake Togo.

Miezi michache iliyopita, kiongozi wa soko la mawasiliano ya simu, Togocom alikuwa ameidhinishwa kulipa zaidi ya faranga bilioni mbili za CFA, sawa na 2% ya mauzo yake ya kila mwaka ya mwaka wa fedha wa 2021<sup>15</sup>, kwa ukiukaji mkubwa wa wajibu wake wa utulivu wa mtandao na upatikanaji wa huduma zake za mawasiliano ya kielektroniki kwa simu, kwa mujibu wa kifungu cha 31 cha sheria ya mawasiliano ya kielektroniki. Vikwazo hivi vinafuata idadi ya ripoti za kielelezo na tafiti za kesi zilizotolewa na Mdhibiti mwaka wa 2022 ili kuhakikisha upatikanaji na ubora wa huduma kutoka kwa waendeshaji wa mawasiliano ya simu.

## USIMAMIZI WA DATA

Katiba ya Togo ya Oktoba 14, 1992, inaweka msingi wa ulinzi wa data na faragha kwa kuhakikisha "inaheshimu faragha, heshima, hadhi na taswira" ya kila raia. Kando na hayo, kifungu cha 29 cha katiba kinasema "Nchi inahakikisha usiri wa mawasiliano. Kila raia ana haki ya usiri wa majibizano yake na mawasiliano yake."<sup>16</sup>

Sheria inayohusu ulinzi wa data binafsi nchini Togo ni Sheria ya Kulinda Data (DPA) n°2019-014 ya Oktoba 29, 2019, inayohusiana na ulinzi wa data binafsi<sup>17</sup>. Inasimamia ukusanyaji, uchakataji, usambazaji, uhifadhi na matumizi ya data binafsi. Inatumika kwa watu binafsi, Serikali, wakazi, makampuni ya kibinafsi na ya umma, na pia uchakataji wa kiotomatiki au usio wa kiotomatiki wa data unaofanywa ndani ya eneo la Togo au katika eneo lolote la mamlaka ambapo sheria za



Togo zinatumika.

Mojawapo ya malengo ya sheria ya ulinzi wa data ni kuwawezesha watu na kuwapa udhibiti wa data zao za kibinafsi. Ina sura inayohusu haki za data za wahusika (watu binafsi) ambayo inajumuisha haki ya ufikiaji, haki ya kurekebisha, haki ya kufuta, haki ya kuzuia, uchakataji, haki ya urahisishaji wa data, haki ya kupinga na haki ya kutokuwa sehemu ya uhusika katika uamuzi unaotokana na uchakataji wa data wa kiotomatiki pekee. DPA ilianzisha kanuni saba za msingi za kushughulikia data binafsi. Kanuni hizi ni pamoja na: kanuni ya ridhaa na uhalali; kanuni ya uhalali na uaminifu; kanuni ya mwisho, umuhimu na uhifadhi; kanuni ya usahihi; kanuni ya uwazi; na kanuni ya usiri na usalama; miongoni mwa nyinginezo.

Sheria hii pia inatoa fursa ya kuundwa kwa wakala wa udhibiti wa ulinzi wa data binafsi, Instance de protection des données à caractère personnel (IPDCP).

Kulingana na sheria, IPDCP itakuwa mamlaka huru ya kiutawala yenye jukumu la kuhakikisha kuwa uchakataji wa data binafsi unafanywa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika sheria.

15 *Autorité de Régulation des communications électroniques...* (2022). Available at: <https://arcep.tg/wp-content/uploads/2022/06/Decision-2022-006-ARCEP-CD-Portant-sanction-TGC-pour-manquement-obligation-de-disponibilite-permanente-continue-et-reguliere-fourniture-des-services-de-CE.pdf> (Accessed: January 25, 2023).

16 Togo 1992 (rev. 2007) constitution (2023) Constitue. Available at: [https://www.constituteproject.org/constitution/Togo\\_2007?lang=en](https://www.constituteproject.org/constitution/Togo_2007?lang=en) (Accessed: January 25, 2023).

17 Journal Officiel du Togo (2020). Available at: [https://www.jo.gouv.tg/sites/default/files/JO/JOS\\_11\\_05\\_2020%20-%2065E%20ANNEE%20N%C2%B0%2016%20BIS.pdf](https://www.jo.gouv.tg/sites/default/files/JO/JOS_11_05_2020%20-%2065E%20ANNEE%20N%C2%B0%2016%20BIS.pdf) (Accessed: January 25, 2023).



Changamoto kuhusu usimamizi wa data nchini Togo inapelekea uanzishwaji wa IPDCP na wanachama wake kuzingatia sheria. Licha ya matangazo ya serikali, chombo bado hakijaundwa.

Changamoto nyingine ni pamoja na mfumo wa kisheria wa data ya utambuzi wa kibayometriki ambao uliwekwa na sheria kuhusu utambulisho wa watu binafsi nchini Togo (Sheria ya e-ID), iliyopigiwa kura mnamo Septemba 3, 2020, na bunge <sup>18</sup>. Sheria mpya, kwa mujibu wa serikali, itaongoza na kudhibiti ukusanyaji wa takwimu za wananchi na serikali. Kwa hivyo, Sheria ya Kitambulisho cha Kibaiyometriki ni sheria ya pili inayosimamia data binafsi. Hata hivyo, bado haijatekelezwa kikamilifu.

### UHURU WA VYOMBO VYA HABARI

Ikiwa na magazeti na majarida 234, vituo vya redio 94 na mitandao kadhaa ya televisheni kwa watu milioni 8.9, Togo ina mazingira mazuri ya vyombo vya habari. Hata hivyo, licha ya wingi wa vyombo vya habari, ikiwa ni pamoja na kuonekana kwa tovuti mpya za mtandaoni katika miaka ya hivi karibuni, wengi wao hufanya kazi chini ya ushawishi mkubwa wa kisiasa.

Tangu 2004, sheria ya vyombo vya habari haitoi tena hukumu za jela kwa ukiukaji, lakini sheria mara nyingi hupuuza. Lugha iliyopitishwa mwaka wa 2020 inahakikisha uhuru wa uandishi wa habari na upatikanaji wa habari kwa wanahabari, kwa sharti la kuheshimu "taarifa nyeti za kiusalama". Upatikanaji wa habari unasalia kuwa mgumu kwa waandishi wa habari, hasa wale kutoka vyombo vya habari vinavyomilikiwa na watu binafsi ambavyo vinakosoa mamlaka. Pia, serikali bado inawafunga wanahabari kwa kutumia vyombo vingine vya kisheria kama vile Kanuni za Jinai za Togo. Mnamo Desemba 2021, Togo iliwashtaki wanahabari wawili ambao walikuwa wakiikosoa serikali kwa "kudharau mamlaka" na "kueneza taarifa za uwongo kwenye mitandao ya kijamii."

Ferdinand Ayite na Joel Egah, wahariri wa jarida la kila wiki la L'Alternative na Fraternite la kila wiki, walikamatwa na kuzuiliwa mnamo Desemba 10, 2021 kutokana na maoni yaliyotolewa wakati wa matangazo ya mtandaoni. Wanahabari hao wawili na msimamizi wao waliachiliwa kutoka gereza la kiraia la Lomé na kuwekwa chini ya uangalizi wa mahakama jioni ya tarehe 31 Desemba 2021. <sup>19</sup> Licha ya kuachiliwa kwao, waandishi hao wawili walikuwa bado wanashitakiwa kwa "kudharau mamlaka" (Kifungu cha 490 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Togo), "kuchafua"



(Kifungu cha 290 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu ya Togo) na "uchochezi wa kuasi mamlaka ya Serikali" (Kifungu cha 495 cha Kanuni hiyo). Joel Egah alifariki wiki chache baadaye kutokana na matatizo ya kiafya kutokana na muda aliokaa jela, familia yake ilisema.

Kumbuka kwamba haki ya uhuru wa kujieleza imeainishwa katika Katiba ya Togo, na pia katika hati kadhaa za kikanda na kimataifa za ulinzi wa haki za binadamu, hasa Kifungu cha 19 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa na Kifungu cha 9 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu. na Haki za Watu, zilizoidhinishwa na Togo mwaka wa 1984 na 1982.

<sup>18</sup> Macdonald, A. (2022) *Togo amends law on biometric identification to advance digital ID ambitions: Biometric Update, Biometric Update* | BiometricUpdate.com. Available at: <https://www.biometricupdate.com/202206/togo-amends-law-on-biometric-identification-to-advance-digital-id-ambitions> (Accessed: January 25, 2023).

<sup>19</sup> *Togo 1992 (rev. 2007) constitution (2023) Constitute*. Available at: [https://www.constituteproject.org/constitution/Togo\\_2007?lang=en](https://www.constituteproject.org/constitution/Togo_2007?lang=en) (Accessed: January 25, 2023).

Kuunganisha mgawanyiko wa kidijitali kupitia elimu Katika kitabu chake “Barua ya Wazi kwa Afrika yenye umri wa miaka hamsini”, “Open letter to fifty-year-old Africa”,<sup>20</sup> mwanasiasa wa Togo na Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Afrika, Edem Kodjo, alizitaka nchi nyingi za Afrika kukumbatia mageuzi ya kidijitali ya bara hilo kwani ndiyo njia pekee ya kuendeleza bara hilo. Nchini Togo, mageuzi ya elimu bado hayajagusa ujumuishaji wa ujuzi wa kidijitali katika mtaala wowote rasmi na hakuna chuo kikuu au taasisi ya elimu ya juu nchini inayofundisha sera ya TEHAMA.

Mnamo mwaka wa 2015, kama sehemu ya mchakato mwingine wa sera ya leapfrog, serikali ilizindua mradi wa majaribio unaoitwa “Ecole Numérique Togo” (ENT), mradi ambao unalenga kuanzisha teknolojia ya dijitali katika elimu na kusisitiza umuhimu wa TEHAMA katika mfumo wa elimu. . Zaidi ya miaka 7 baadaye, hakuna ripoti ya matokeo inayopatikana katika awamu ya majaribio na zaidi ya wanafunzi 1,548 876 na zaidi ya wanafunzi 85,000 bado hawanufaiki na mitaala ya TEHAMA. Moja ya sababu za kudorora kwa elimu nchini Togo, na hasa kuhusu tehama, ni ufadhili. Hata hivyo, serikali imepata msaada wa faranga za CFA bilioni 15 kutoka Benki ya Dunia ili kuunga mkono mpango wa ENT ambao haujaweka sera, ramani au mtazamo wowote kuhusu jinsi serikali inatarajia kuanzisha TEHAMA katika mitaala ya elimu.

Kuanzisha mitaala ya TEHAMA katika shule za Togo sasa ni dharura kwani bara zima linaelekea kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda. Katika miaka ya 2000, mgawanyiko wa kidijitali nchini Togo ulikuwa mkubwa. Lakini katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, kukiwa na kiwango cha kupenya kwa mtandao wa intaneti cha zaidi ya 90%, na watumiaji wa mtandao milioni 2.23, ni muhimu sana kuchunguza maeneo mengine ya ufadhili ili kuunga mkono azma hiyo zaidi ya misaada ya kimataifa, ufadhili wa wafadhili na mikopo.

## **MFUKO WA HUDUMA NA UPATAJI KWA WOTE (USAF)**

Mfuko wa Huduma na Upataji kwa Wote (USAF), utaratibu wa ufadhili wa kupata michango, kwa kawaida kutoka kwa waendeshaji wa mtandao wa mawasiliano, ili kuchangia katika kuhakikisha kuwa huduma za TEHAMA zinapatikana na kumudu bei

nafuu kwa watu wengi iwezekanavyo, imekuwa muhimu katika kufadhili ujumuishaji wa kidijitali na miradi ya elimu ya kidijitali.

Katika nchi nyingine katika bara hili, fedha hizi pia ni muhimu kwa maana kwamba zina ushawishi mkubwa juu ya uzoefu wa mtandaoni wa umma uliotengwa katika nchi.

Pamoja na kwamba mdhibiti ametaja matumizi ya mfuko katika ripoti zake za mwaka, hakuna taarifa ya matokeo au uwazi kuhusu mchakato na miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Mfuko. Mdhibiti ndiye anayesimamia utekelezaji wa miradi chini ya mfuko huo kwa usimamizi kutoka kwa wizara ya TEHAMA.

Nchini Togo, mkazo wa mfuko tangu kuanzishwa kwake mwaka 1998 umejikita katika upatikanaji wa huduma ya simu ya ‘sauti’ na sehemu za kufikia katika maeneo ya vijijini. Miaka 20 baadaye, mwaka wa 2018, serikali ilipitisha agizo la kupanua huduma hiyo kuelekea miradi ya ujumuishaji wa mtandao mpana na dijitali kwa jamii ambazo hazijahudumiwa ili kuunganisha 95% ya watu.



## **MAPENDEKEZO NA HATUA ZA KUCHUKULIWA:**

### **KWA SERIKALI:**

Serikali lazima ianzishe mchakato wa wadau

20 Kodjo, E. (2010) *Lettre Ouverte à l'Afrique Cinquantenaire*. Paris: Editions Gallimard.

mbalimbali wa sera, sheria na kanuni zikiwemo asasi za kiraia (CSOs), wasomi na jumuiya ya kiufundi.

Serikali lazima ilinde uhuru wa kujieleza, ufikiaji wa habari mtandaoni na nje ya mtandao. Serikali, mamlaka za udhibiti wa mawasiliano na makampuni ya simu lazima zidumishe ufikiaji wa mawasiliano ya simu, huduma za intaneti, mifumo ya kidijitali, na teknolojia za kukwepa, hasa wakati wa uchaguzi, maandamano na vipindi vya migogoro. Kukatizwa kimakusudi kwa ufikiaji wa mtandao na huduma za mtandaoni huathiri haki za watu binafsi za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiraia.

Serikali lazima izingatie kanuni za haki za binadamu, uwazi na usimamizi wa kidemokrasia katika sheria zinazodhibiti maudhui ya mtandaoni nchini Togo. Serikali inapaswa kuepuka kuzuia au kuweka masharti magumu ya udhibiti kwenye mitandao ya jumuiya, na kuweka marufuku ya moja kwa moja au ya kiholela kwenye mitandao ya kijamii na majukwaa ya ujumbe.

Kupitia USAF, serikali na mdhibiti wanapaswa kuwa na uwezo wa kupanua muunganisho, kuunda mahitaji ya ziada ya ufikiaji wa mtandao, kusaidia nguzo zilizopo za uchumi wa nchi, na kutoa bidhaa mbalimbali za kijamii na huduma za serikali.

Kupitia USAF kwa kipaumbele cha ufikiaji jumuishi wa mtandao, serikali na mdhibiti lazima wafadhili uunganisho kwa wale walio pembezoni, kama vile wanaoishi vijijini na wanawake na wasichana.

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine lazima iunde chombo jumuishi na kamati ya wadau mbalimbali ili kusimamia USAF ili kusaidia kufikia malengo ya ngazi ya juu ya kiserikali na kusaidia maendeleo ya jumla ya uchumi wa nchi.

Serikali lazima iunge mkono vyombo vya habari vya mtandaoni na kukuza nafasi ya habari dhabiti. Kupambana na habari potofu na propaganda huanza na ufikiaji wa umma kwa habari ya kuaminika na kuripoti kutoka kwenye matukio.

Serikali na wadau lazima waunganishe kikamilifu kanuni za haki za binadamu katika utekelezaji wa sera za ushindani na kuhimiza uwekezaji mpya katika tasnia ya mawasiliano.

Serikali lazima ishughulikie mgawanyiko wa kidijitali. Ufikiaji usio sawa wa mtandao huchangia ukosefu wa usawa wa kiuchumi na kijamii na hudhoofisha manufaa ya mtandao wa bure na wazi. Kwa muda mfupi, serikali zinapaswa kufanya kazi

na watoa huduma ili kuinua ukomo wa data.

### **KWA JUMUIYA YA KIRAIA:**

Mashirika ya kiraia lazima yatetee kuachiliwa mara moja, bila masharti kwa wale waliofungwa kwa kujieleza mtandaoni unaolindwa na viwango vya kimataifa na kuhimiza hatua za kurekebisha.

Mashirika ya kiraia lazima yafanye uchanganuzi wa maonyo ya mapema kuhusu mbinu za kuingilia uchaguzi zinazoweza kutokea wakati wa chaguzi za mitaa na chaguzi kuu, na kuhamasisha kampeni za utetezi ili kuzuia athari mbaya.

### **KWA SEKTA YA KIBINAFSI:**

Kampuni lazima zishiriki katika mazungumzo endelevu na mashirika ya kiraia ili kuelewa athari za sera na bidhaa za kampuni na mahitaji ya watumiaji.



     @ParadigmHQ

[www.paradigmhq.org](http://www.paradigmhq.org)

Hakimiliki © 2023